

Maswali

1. Yesu alienda wapi?
2. Nani alikuwa amekaa kando ya barabara?
3. Mbona Bartimayo alikuwa akiomba?
4. Siku moja Bartimayo alisikia nini?
5. Bartimayo alifanya nini aliposikia Yesu anakuja?
6. Yesu aliambia wanafunzi wake wafanye nini?
7. Bartimayo alitupa nini?
8. Bartimayo aliuliza Yesu amfanyie nini?
9. Mbona Yesu alisema kwamba Bartimayo alikuwa amepona?
10. Bartimayo alifanya nini alipoona kwamba amepona?

Majibu

1. Yesu alikuwa anaenda Yeriko.
2. Bartimayo alikuwa amekaa kando ya barabara.
3. Alikuwa akiomba omba kwa sababu alikuwa kipofu na hange-weza kufanya kazi.
4. Alisikia umati wa watu ukikuja.
5. Alipaza sauti, “Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu.”
6. Yesu aliambia wanafunzi wake wamletee Bartimayo.
7. Bartimayo alitupa joho lake.
8. Aliuliza Yesu amsaidie apate kuona.
9. Yesu alisema kwamba alipona kwa sababu alikuwa na imani.
10. Alikimbia barabarani akisifu Mungu akiambia kila mtu chenye Yesu amemfanyia.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



43 Bartimayo kipofu

Marejeo

Marko 10: 46 -52

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Bartimayo alikuwa na imani kuwa Yesu angemponya. Yesu alimponya kwa sababu alikuwa na imani.

Maneno maalum

- 43.1 Yesu + Yeriko + kipofu + Bartimayo + omba omba
- 43.2 Umati + Yesu + Bartimayo anachangamka + Yesu + mmlete hapa
- 43.3 Amka haraka + Bartimayo + wanafunzi + enda kwa Yesu + unataka nini? + nione + imani imekufanya uone + Yesu aliponya
- 43.4 Bartimayo + ona + maua, miti, uso wa Yesu + kimbia barabara mrefu +sifu Mungu +kila mtu anafurahi

43.1 Yesu alikuwa na safari ya kwenda Yerusalemu. Hapo njiani alipitia Yeriko. Enje ya mji wa Yeriko kulikuwa na mtu kipofu aliyeitwa Bartimayo. Alikaa kando ya barabara akiomba chakula na pesa. Watu waliokuwa wakarimu walimpa pesa lakini hawakumpa kitu cha dhamana sana – uwezo wa kuona.



Kila siku maskini Bartimayo alikaa kando ya barabara akiomba. Masikio yake ilisikia vishindo vya miguu ya watu haraka sana na alijua vishindo vya miguu ya marafiki na ile ya wasio marafiki. Alisikia sauti ya chini sana yenye mimi na wewe hatungesikia.

43.2 Siku moja alisikia sauti ya vishindo vya miguu ya umati wa watu wengi sana. Aliuliza mtu aliyekuwa akipita kwamba kulikuwa na nini. Aliambiwa kwamba Yesu wa Nazareti alikuwa anakujia kwa hiyo barabara. Aliposikia hivyo, alifurahi sana na kuita, “Yesu, Mwana wa Daudi, unirehemu.”

Yesu alisimama na akaambia wanafunzi wamletee yule kipofu.

43.3 Wanafunzi walienda kwa Bartimayo na wakamwambia, “Amka haraka, Yesu anakuita.” Bartimayo aliamka haraka akatupa kando joho lake mzee. Wanafunzi walimwongoza mpaka penye Yesu alikuwa amesimama.

Yesu alimwambia, “Unataka mimi nikufanyie nini?” Unaweza kubahadisha ni nini maskini Bartimayo angetaka zaidi kuliko kitu kingine chochote. Alisema, “Bwana, tafadhali nipate kuona.” Yesu alimjibu, “Imani yako imekufanya kuona.” Halafu Yesu akamponya, kwa hivyo Bartimayo hakukuwa kipofu tena.

43.4 Papo hapo macho yake ilifunguka na akaanza kuona. Akaona maua, miti, mawingu angani na vingine. Lakini zaidi ya yote, aliona uso mkarimu wa Yesu. Alijazwa na furaha, akakimbia barabarani akiambia watu wote chenye Yesu alikuwa amemfanyia. Watu wote walisifu Mungu pia, kwa sababu walimwona maskini Bartimayo amepata kuona.

